



## TAARIFA KWA UMMA

Dar es Salaam- 3 Februari, 2020

### **Uwasilishaji wa Taarifa za Maandalizi ya Maonesho na Misafara ya Kibiashara itakayofanyika Ndani na Nje ya Nchi kwa mwaka 2020**

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inapenda kuwakumbusha Waandaji wa Maonesho na Misafara ya Kibiashara Ndani na Nje ya Nchi, Wamiliki wa Kumbi za Maonesho, Wizara, Taasisi za Umma na Binafsi pamoja na Wadau wote kwa ujumla kuwa wanatakiwa kuwasilisha Taarifa za Maandalizi ya Maonesho na Misafara mbalimbali ya Kibiashara Ndani na Nje ya Nchi kwa mwaka 2020.

Taarifa za maandalizi ya shughuli hizo za kibiashara zinatakiwa kuwasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) miezi mitatu kabla ya kuanza kuratibu maandalizi yake.

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Na. 4 ya 2009 kimeainisha Majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na TanTrade. Pamoja na mengine, TanTrade ina jukumu la Kuunganisha na Kudhibiti Soko la Ndani ikiwa ni pamoja na kudhibiti Maonesho pamoja na Misafara ya Kibiashara kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 5(1) (b) cha Sheria hiyo.

Aidha, TanTrade ina Mamlaka ya kutoa Vibali mbalimbali kwa Waandaji wa Maonesho na Misafara ya Kibiashara (Aya ya 3 (1)(k) ya Kanuni za Sheria za TanTrade, 2010), kabla ya shughuli husika kufanyika.

TanTrade inatoa Rai kwa Waandaji wa Maonesho na Misafara ya Kibiashara Nchini kuwasilisha Taarifa za Maonesho, Misafara ama Shughuli nyingine za Kibiashara; na kutimiza masharti yote ya maandalizi ya Shughuli hizo kama yalivyoainishwa katika Sheria. Kwenda kinyume na masharti hayo ni kosa kisheria na adhabu kali zitatolewa dhidi ya mtu huyo.

**Imetolewa na;**

Theresa H. Chilambo  
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano**